# MKATABA WA UNUNUZI WA SAMANI ( FURNITURE) JENGO LA

# TELEMEDICINE

# MKATABA NAMBA

# ME/007/SRRH/2021/2022/ G/03

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**


**MKOA WA SINGIDA.**
**Anwani ya simu: "AFYA"**
**Simu Na. 026 - 2502397**
**Nukushi Na. 2502360**
**Barua pepe:**singidarrhafya.go.tz

**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA,**
**S.L.P 104,**
**SINGIDA.**


## MKATABA WA UNUNUZI WA SAMANI (FURNITURE) JENGO LA TELEMEDICINE KATIKA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA SINGIDA ENEO LA MANDEWA NAMBA YA MKATABA (CONTRACT NO) ME/007/SRRH/2021/2022/G/03

Mkataba huu umefanyika hapa Singida leo hii tarehe 03 mwezi Januari Mwaka 2022.

**KATI YA**

**MGANGA MFAWIDHI HOSPITALI YA RUFAA MKOA WA SINGIDA** (Ambaye katika mkataba huu atajulikana kama **MNUNUZI**) kwa upande mmoja.

**NA**

**MOHAMED FAKIH BAKARI(PENJEWANI GENERAL SUPPLIES & ELECTRONICS)** (Ambaye katika mkataba huu atajulikana kama **MZABUNI** kwa upande mwingine).

**KWAKUWA, MNUNUZI** anahitaji **SAMANI** kwa ajili ya ya matumizi ya jengo la "telemedicine" kwa ajili ya kutolea huduma ya tiba mtandao kwa gharama ya **shilingi 8,400,000/= (Milioni nane na laki nne) tu** Pamoja na ongezeko la thamani(**VAT)**

**KWAKUWA, MZABUNI** tajwa hapo juu yuko tayari kumuuzia **MNUNUZI** samani tajwa hapo juu kwa bei iliyoainishwa kwenye "ploforma invoice"
**NA KWAKUWA, MNUNUZI** kwa hiari yake mwenyewe amekubali kununua samani tajwa hapo juu kwa bei iliyoainishwa kwenye "ploforma invoice"
**Pande zote mbili zimekubaliana kama inavyoonekana hapo chini:-**

1. Kwamba, **MNUNUZI** atamlipa **MZABUNI** fedha kiasi cha shilling 8,400,000/= (**Mililioni nane na laki nne) tu** Pamoja na ongezeko la thamani **(VAT)** baada ya kamati ya mapokezi kupoke na kujiridhisha na ubora wa samani zifuatavyo kwa ajili ya matumizi yaliyokusudiwa; Conference table, Executive chair na Computer table.
2. Kwamba, hakutakuwa na malipo ya awali katika Mkataba huu.

3. Kwamba, mkataba huu utaanza kutekelezwa mara baada ya kuwekwa saini na pande zote mbili na utafikia ukomo mara tu baada ya kutekelezwa na kukamilika kwa kazi husika kama ambavyo pande zote mbili zilivyokubaliana.
4. Kwamba, upande wowote unaweza kuvunja mkataba huu kwa kutoa notisi au taarifa ya maandishi ya siku 3 ya kusudio la kuvunja mkataba kwa upande mwingine endapo upande mwingine utashindwa kutekeleza masharti ya mkataba huu.
5. Kwamba, mkataba huu utatafsiriwa kwa mujibuwa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**KWA KUSHUHUDIA** haya wahusika wa makubaliano haya wametia sahihi zao kwa namna na katika siku na tarehe kama inavyoonekana hapa chini;

Imetiwa sahihi Singida Mjini na **MGANGA MFAWIDHI HOSPITALI YA RUFAA MKOA WA SINGIDA** ambaye namfahamu/~~ametambulishwa kwangu na~~ ........................................................................ ambaye namfahamu leo tarehe ......03...... mwezi Januari, 2022.

**MNUNUZI**

MGANGA MFAWIDHI HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA SINGIDA

**MBELE YANGU:**

JINA....DKT. DEOGRATIAS G. BANUBA.

SAHIHI....................................

ANUANI.......S.L.P 104..................

WADHIFA.......MGANGA MFAWIDHI.

**MBELE YANGU:**

JINA.........RADHIA HAMIS..................

SAHIHI..............................................

ANUANI.................219 SINGIDA............

WADHIFA.................WAKILI.................

Imetiwa sahihi Singida Mjini na **MOHAMED FAKIH BAKARI (PENJEWANI GENERAL SUPPLIES & ELECTRONICS** ambaye namfahamu binafsi/ametambulishwa ~~ametambulishwa kwangu na~~.........................ambaye namfahamu leo tarehe.......03...... mwezi January 2022

**MZABUNI**

PENJEWANI GENERAL SUPPLIES AND ELECTRONICS P.O. Box 102 SINGIDA

**MBELE YANGU:**

JINA.........RADHIA HAMIS..................

SAHIHI..............................................

ANUANI.................219 SINGIDA............

WADHIFA.................WAKILI.................